Mwongozo wa Utafiti wa Kibiblia

# Miguuni Pake Yesu



Ngazi ya 1

Miguuni Pake Yesu

# Kielezo cha Mada ya Mwongozo wa Utafiti wa Kibiblia

## Ngazi ya I

- ❑ 1 Tajiri Asiyejitambua
- ❑ 2 Je, Yawezekana Kuufahamu Wakati Ujao?
- ❑ 3 Chanzo cha Maumivu Mengi ni Nini?
- ❑ 4 Hatua Nne Kuelekea kwenye Amani ya Ndani na Furaha
- ❑ 5 Namna ya Kuboresha Utu Wetu
- ❑ 6 Ufumbuzi Bora Zaidi kwenye Matatizo na Yanayonihusu
- ❑ 7 Je, Ni Nani Atakayeitawala Dunia Hatimaye?
- ❑ 8 Sababu za Mashaka ya Dunia Yaliyopo
- ❑ 9 Tukio Kubwa Zaidi la Milenia ya Tatu

## Ngazi ya 2


- ❑ 10 Siri ya lile Sanduku la Dhahabu la Agano
- ❑ 11 Mfumo wa Maisha Unaoleta Usalama na Amani
- ❑ 12 Kumi Kutoa Moja ni Sifuri
- ❑ 12a Kioo na Kivuli
- ❑ 13 Njia Bora Zaidi ya Kuushinda Msongo
- ❑ 14 Udanganyifu Mbaya Zaidi katika Historia
- ❑ 15 Viwango Viwili vya Upendo
- ❑ 16 Je, Kuna Maisha baada Kifo?
- ❑ 17 Ushauri wa Kimbingu dhidi ya Nguvu Zisizoelezeka
- ❑ 18 Kitabu cha Ufunuo na Hatima ya Sayari Yetu
- ❑ 19 Maono Juu ya Ulimwengu Ulio Bora Zaidi

## Ngazi ya 3

- ❑ 20 Je, Mpinga Kristo Yupo Tayari?
- ❑ 21 Unabii wa Kushangaza wa Miaka 2,300
- ❑ 22 Utetezi Wangu Mbele ya ile Mahakama Kuu
- ❑ 23 Je, ni Kwa Nini Kumekuwako na Dini Nyingi Sana?
- ❑ 24 666 na Marekani Katika Unabii
- ❑ 25 Siku ya Muhimu Zaidi Katika Maisha ya Mtu
- ❑ 26 Namna ya Kumtambua Nabii wa Kweli
- ❑ 27 Funguo Saba Kwenye Maisha ya Kiafya
- ❑ 28 Namna ya Kutatua Matatizo Yangu ya Kifedha
- ❑ 29 Uzuri Halisi
- ❑ 30 Siri ya Mafanikio



# 1 TAJIRI ASIYEJITAMBUA



## *Je, ulifahamu ya kwamba unayo hazina kubwa?*

Ulipewa na Mungu Mwenyewe, na lengo lake ni kukufanya wewe uwe na furaha. Tunaongea juu ya Maandiko Matakatifu.

***Je, ni kwa nini Biblia ichukuliwe kama hazina?***

*Ni kwa sababu inazo ahadi 31,000 pamoja na ushauri makini katika familia, vijana, pamoja na elimu. Inatutia nguvu, inatufariji, na kutuimarisha. Inatuambia "Usiogope" kwa mara 360.*

**Biblia inaitwa pia kama:**

Maandiko Matakatifu, Neno la Mungu, Kitabu Kitakatifu, Waraka wa Kimbingu, Kitabu cha Vitabu.

**1. Je, Mungu anafunua nini katika Biblia? Amosi 3:7.** ______________________________

*Neno hili Biblia linamaanisha "seti ya vitabu." Kuna jumla ya vitabu 66: 39 katika Agano la Kale na 27 katika Agano Jipya.*

## *CHIMBUKO LA BIBLIA*

**2. Wanadamu waliipataje Biblia? 2 Timotheo 3:16.**

*Maandiko Matakatifu yali* ________________________________ *na Mungu.*

**3. Je, ni nani aliyeyavuvia mawazo ya wanadamu wale? 2 Petro 1:21.**

________________________________________________________________

**4. Kwa hiyo, Twaweza kuiitaje Biblia? 1 Wathesalonike 2:13.**

________________________________________________________________

**5. Je, ni ushahidi gani uliopo unaotueleza kwamba Biblia ilivuviwa na Mungu?**

*a)* ***Ulinganifu wa ujumbe wake****, ijapokuwa iliandikwa na waandishi zaidi ya 40 kwa kipindi kinachozidi miaka 1600, inatuletea ujumbe uliounganika. Watu hawa walitoka katika namna mbali mbali za maisha. Miongoni mwao walikuwa ni: wafalme, mawaziri wakuu, madaktari, wavuvi wa samaki, wachungaji wa mifugo, manabii.*

*b)* ***Usahihi wake wa kihistoria, uliothibitishwa na wataalamu wa mambo ya kale****.*
- *Magunduzi mengi yaliyofanyika katika Mashariki ya Kati yanaithibitisha historia ya Biblia kuwa ni ya kushangaza.*
- *Majiji kama vile Lachish, Tel Hazor, Megiddo, Ninawi pamoja na mingineyo, sehemu ambazo zilikuwa zisizofahamika, zimefukuliwa na wataalamu wa mambo ya kale.*

*c)* ***Zaidi ya nabii 2,300 zimetimilika kwa usahihi:***
- *Inafurahisha kwamba nabii zilizotaja juu ya falme kama vile Babeli, Tiro, Sidoni, Misri, pamoja na mataifa kama lile la Wayahudi.*
- *Ndani yake kuna matabirio juu ya maendeleo ya kisayansi. Yanataja juu ya magari pamoja na eropleni, zile sheria za uvutano, uzito wa hewa, mviringo wa dunia, n.k., kinyume na maarifa ya wakati ule.*
- *Kupitia kwa miunganiko mbali mbali ya kinabii katika Kitabu cha Ufunuo, historia ya kiutawala na kidini katika miaka ile 2,000, imeelezwa hapa. Humu tumeelezwa kama ni kwa*

*nini Hitler pamoja na Napoleoni walishindwa vitani, ni nani atakayeitawala dunia, sababu ya hatari zilizopo duniani hivi sasa, n.k.*

- *Kuna nabii 333 juu ya mtu fulani, nabii ambazo ziliandikwa karne kadha kabla hata hajazaliwa.*

**d) Usahihi wa jumbe zake.** *Mfano wake ukiwa ni zile Amri Kumi.*

**e) Watu walioongolewa nayo.**

**6. Ni nani aliye mada yake kuu?**

*Mada kuu ya Biblia ni mtu yule wa pekee: Yesu Kristo.*

- *Ametajwa chini ya majina zaidi ya 2000 ili kuziangazia sifa Zake.*
- *Matabirio 333 yalionyesha juu ya maisha na utume Wake kabla hajazaliwa bado.*
- *Agano Jipya ndilo linafafanua juu ya utimilizo wa matabirio haya.*

## KUSUDI LA BIBLIA

**7. Je, tunapata nini kutokana na kuichunguza Biblia? 2 Timotheo 3:15.**

___________________________________________

**8. Tunayo Biblia kwa ajili gani? 2 Timotheo 3:16 -17.**

___________________________________________

**9. Je, Biblia inatupatia nini sisi?**

*a) Warumi 15:4.* ________________ *b) Yeremia 15:16.* ________________

**10. Ili kutusaidia sisi kuyafahamu maadili yake, Biblia inalinganishwa na nini na kwa sababu gani?**

*a) Nuru. Zaburi 119:105. Inai*________________ *njia yetu.*

*b) Upanga. Waebrania 4:12. Inatu*________________ *sisi dhidi ya makosa.*

*c) Mkate. Mathayo 4:4. Ina*________________ *maisha yetu ya kiroho.*

*d) Moto na nyundo. Yeremia 23:29.*

*Moto* ________________ *na nyundo* ________________

*e) Maziwa. 1 Petro 2:2. Inatusaidia sisi* ________________ *kiroho.*

*f) Kioo. Yakobo 1:23. Ina* ________________ *sisi kasoro zetu.*

*g) Barua. Ina* ________________ *sisi juu ya upendo Wake kwetu.*

## CFUNGUO TANO ILI KUIELEWA BIBLIA

**1. Tuichunguze Biblia kwa namna gani? Matendo 17:11.**

___________________________________________

**2. Yatupasa tuhiari kufanya nini? Yohana 7:17**

___________________________________________

**3. Je, ni njia ipi iliyo na tija zaidi; ni kwa kuchunguza ama kusoma mada mbali mbali, kulinganisha mafungu haya na yale mengine pekee? Isaya 28: 20.**

___________________________________________

**4. Je, tunashauriwa kupokea maelekezo ya Biblia kutoka kwa watu wengine? Mathayo 28:20** ___________________________________________

**5. Je, tufanyeje kabla hatujaingia kwenye kuyachunguza Maandiko? Yakobo 1:5.**

___________________________________________________________________________

## *HITIMISHO*

**11. Je, Biblia ilipata kuzuiwa kutokana na mapingamizi mengi yaliyoikabili? Isaya 40:8.**

*Neno la Mungu* ___________________________________________________________ .

**12. Ushauri wa Yesu ulisemaje? Yohana 5:39.**

___________________________________________________________________________

**13. Mtu anayejifunza Neno la Mungu anapasa kufikiria nini? Ufunuo 1:3.**

___________________________________________________________________________

***Uamuzi wangu:*** *NInaamini ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa, nami ninaazimia kui-chunguza kila siku.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana* ❑ *Nahitaji maelekezo zaidi*

# 2 *JE, YAWEZEKANA KUUFAHAMU WAKATI UJAO?*



Mara zote watu wametamani kuufahamu wakati ujao. Mamilioni ya watu huagua kwa kutazama nyota kila siku. Wanasiasa wengi, wafanya biashara pamoja na wasanii huwategemea wapiga ramli ili kufanya maamuzi muhimu. Je, wanaelezwa kilicho kweli?

Kuufahmu wakati ujao ni sifa ya pekee inayomhusu Mungu wa kweli! Isaya 46:9, 10; 42:9.

Yeye huwavuvia manabii. Yeye Ndiye Mtoaji halisi wa Maandiko Matakatifu.

Usahihi wa uvuvio wa kimbingu ni kutimilika kwa unabii huo. Katika fundisho hili, tutajifunza juu ya nabii zilizo muhimu sana. Tuziangalie hizi chache kama mfano.

Tuwe nao uzoefu katika nabii zipatazo 2,300 zilizomo katika Biblia.

## *MIJI ILIYOLAANIWA*

Mji wa Tiro, ulio katika Asia Ndogo, ulikuwa ni mji tajiri sana. Ulifanya biashara pamoja na nchi nyingine nyingi pamoja na utajiri wake mwingi; dhambi, uasherati, kiburi, ibada za miungu, na uovu pia viliongezeka.

Wakazi wake walifurahia pale mji wa Yerusalemu ulipoangamizwa na Nebukadreza nao wakalisahau lile agano walilolifanya pamoja na mfalme Daudi, na kulipeleka taifa lote utumwani. (Amosi 1:9,10). Matokeo ya jambo hili ….

1. **Je, ni unabii gani uliotolewa kuuhusu mji huu? Ezekieli 26:3-9; 12-14.**

   *Taja mambo matatu yaliyokugusa zaidi juu ya unabii huu.*

   ________________________________________

   ________________________________________

   ________________________________________

   *Utimilizo wa unabii huu: Nebukadreza aliuzingira mji wa Tiro kwa vita kwa miaka 13 na kisha akautelekeza. Baadaye, wakazi wake wakakimbilia sehemu iliyokuwa ni kisiwa cha mji ule. Miaka 200 baadaye, Alexanda Mkuu alijenga boma la kuzuwia maji kutokea kwenye mawe yake ya kutomelea, na hata vumbi lake lilitupwa baharini. Katika miezi 7, aliweza kukipiga kisiwa kile cha Tiro. Haukujengwa tena.*

2. **Je, ni neno gani lililotabiriwa juu ya Yerusalemu? Mathayo 23:37, 38; 24:1, 2.**

   ________________________________________

   *Unabii huu ulitimilika mnamo mwaka wa 70 B.K.*

3. **Je, Misri ingelinganishwaje na mataifa mengine baada ya kufanywa kuwa taifa lenye nguvu kwa miaka elfu kadha? Ezekieli 29: 9, 15.**

   ________________________________________

4. **Je, ni adhabu gani ilitabiriwa juu ya Wayahudi kutokana na kutomtii Mungu? Kumbukumbu 28:15, 25, 37.**

   ________________________________________

## *MAGUNDUZI YA KISASA NA MABUNIFU YALITABIRIWA MIAKA 3,500 ILIYOPITA*

**5. Je, Biblia ilisema nini juu ya dunia hii pale watu walipodhani kuwa imetegemezwa na tembo wakubwa? Ayubu 26:7.**

___________________________________________________________________________

*Biblia pia inataja kuwa dunia ni ya duara (Isaya 40:22). Neno chug, katika Kiebrania, humaanisha mviringo.*

**6. Katika Ayubu 28:25, twasoma juu ya uzito wa hewa. Je, kumeandikwa nini juu ya mikondo ya upepo na mihula ya maji? Muhubiri 1:6, 7.**

___________________________________________________________________________

**7. Je, Biblia inasemaje juu ya idadi ya nyota, katika wakati fulani nyota zilipohesabiwa? Yeremia 33:22.** ______________________________________________

**8. Biblia na afya.**

*a) **Mbinu za vitakasa.** (Hesabu 19:13, 7). Watu walipasa kusafisha mikono yao baada ya kugusa maiti.*

*b) **Tohara katika siku ya 8** (Mwanzo 17:12). Imegunduliwa ya kwamba vitamini K na madini ya Prothrombin, vitu viwili vya asili ambavyo huchangia katika kuganda kwa damu, hufikia kilele cha juu zaidi panapo siku ya 8 maishani.*

**Magonjwa ya kiakili:**

**9. Moyo wenye furaha ukoje? Mithali 14:30; 17:22.**

___________________________________________________________________________

**10. Mafungu haya mawili yanatuelekeza kwenye mavumbuzi gani ya kisasa?**

*a) Isaya 60:8.* ____________________________

*b) Nahumu 2:4.* ____________________________

## *MATABIIRIO 333 KUMHUSU KRISTO, yaliyoandikwa miaka 600 – 1600 kabla ya kuzaliwa Kwake*

**11. Kristo angezaliwa wapi? Mika 5:2.**

___________________________________________________________________________

*Kristo angekuwa wa uzao wa Daudi. (Yeremia 23:5, 6). - Wa Ibrahimu. (Mwanzo 22:18). – Wa kabila la Yuda. (Mwanzo 49:10).*

**12. Je, ni mwanamke wa namna gani ambaye angemzaa mwana wa Mungu? Isaya 7:14.**

___________________________________________________________________________

**13. Taja sifa nne za tabia ama utumishi Wake. Isaya 42:1-4, 6, 7.**

*a)* ____________________________ *b)* ____________________________

*c)* ____________________________ *d)* ____________________________

**14. Kwa kulingana na unabii, je, ni kima gani kingelipwa kwa kumsaliti Kristo? Zekaria 11:12.**

___________________________________________________________________________

**15. Je, unabii wa Isaya, ulioandikwa miaka 700 kabla, unasema nini juu ya maisha, mateso na kifo cha Yesu? Isaya 53:1-12.**

*a) Je, ni wangapi waliomngojea?* ______________________________________________

*b)* *Naye alitendewaje?* ____________________________________________________________

*c)* *Je, alijitwalia nini juu Yake Mwenyewe?* ___________________________________________

*d)* *Je, amefananishwa na tabia ya mnyama gani?* _______________________________________

## HITIMISHO

Unabii unaomhusu Kristo ni ushahidi usiokanushika ya kwamba alikuwa ni Mwana wa Mungu. Matabirio mengi katika Biblia, ambayo yametimilika tayari, ni ushahidi ya kwamba haya ni NENO LA MUNGU. Mungu anaahidi mafanikio kwao wale wanaowaamini manabii Wake. 2 Nyakati 20:20.

Je, unaamini juu ya hili ama bado una mashaka?

---

***Uamuzi wangu:*** *NInaamini ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa, nami ninaazimia kuichunguza kila siku.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana* ❑ *Nahitaji maelekezo zaidi*

---

# 3 CHANZO CHA MAUMIVU HAYA MENGI NI NINI?



Matokeo ya yale mabomu yaliyopigwa katika ile vita ya dunia iliyopita, maelfu ya watu waliachwa bila ya makazi.

Mara nyingi watoto walizagaa katika mitaa wakiwatafuta wazazi wao. Wengi wao hawakuweza kuwapata, kwa kuwa aidha walikuwa wamekufa ama ule ukatili wa vita uliwatenga mbali. Pale nyumbani, mahali ambapo ndipo wangepatikana, hawakuwapo tena.

Yote ya mwanadamu ni vurugu tupu. Kuna kitu kilichotokea ambacho kimewafanya kupoteza mwendo wao halisi. Badala ya furaha, tunakutana na hali ya kufadhaika; badala ya kuishi salama, tunakutana na masumbufu. Je, ni kwa nini yule asiye na hatia ateseke? Je, ni kwa nini maumivu, magonjwa na kifo vimekuwapo? Je, Mungu aliiumba dunia yenye maovu? Asili yetu halisi pamoja na hatima yake ni ipi? Sisi tumetoka wapi, nasi twaenda wapi? Haya ndio maswali ambayo yanawakalia watu wengi lakini ni Mtoaji wa uzima pekee ndiye anaweza kutoa jibu.

## *CHIMBUKO LA MWANADAMU*

1. **Mungu ni Bwana, Naye alikuwako kabla ya kitu cho chote hakijaumbwa. Vitu vyote viliumbwa na Yeye (Mwanzo 1:1). Lakini Biblia inamaanisha nini, pale inaposema katika wingi "Na tufanye", katika Mwanzo 1:26?**

   *a) Baba wa mbinguni. (Waefeso 4:6).* *b) Mwana, Yesu Kristo. (Yohana 1:1-4).*

   *c) Roho Mtakatifu. (Yohana 14:26).*

   Ukurasa wa kwanza wa Biblia unatuelekeza kunako nafsi tatu za Uungu. Mistari kadha ya Maandiko yanataja uwapo wa Kristo katika majukumu Yake katika uumbaji wa dunia hii. (Wakolosai 1:15-17; Waebrania 1:1-3; 8-10).

2. **Je, mwanadamu aliumbwaje? Muhubiri 7:29.** ______________________________

3. **Mwanadamu alipewa karama nne kutoka kwa Muumbaji wake.**
   a) **Uzima wa milele**. Mwanadamu hakuhukumiwa kifo.
   b) **Tabia ya haki.** Dhambi haikuwamo ndani yake.
   c) **Maskani nzuri.** Maumivu na magonjwa hayakuwapo.
   d) **Utawala juu ya kila kitu.** Adamu alikuwa ndiye kito cha taji ya uumbaji. Asili yote ilikuwa chini ya utawala wake.

4. **Sharti la pekee alililopewa ili kwamba hali hii ibaki hivi ni lipi? (Mwanzo 2:16, 17).**

   ______________________________________________

   *Kwa ajili ya furaha yake, alipasa kujifunza kutii. Je, kunaweza kuwako na furaha nyumbani iwapo wazazi hawaheshimiwi, ama utaratibu katika taifa utaendaje iwapo serikali haiheshimiwi? Ile sheria ya Mungu iliwekwa moyoni mwa mwanadamu tangia mwanzo. Ilikuwa ndio msingi wa serikali ya Mungu.*

5. **Mwanadamu akaamua kumtii bwana mwingine – Shetani, mfalme wa giza, akamshawishi. Je, Mungu alimuumba yule "mwovu"? Hapo mwanzo Shetani alikuwa nani? Ezekieli 28:13-17.**

   *Alikuwa ni* ______________________ *ambaye* ______________________ *dhidi ya Mungu.*

6. **Mwanadamu akaja kuwa nani pale alipokubali kushindwa na Shetani? 2 Petro 2:19; (Warumi 6:16).** ______________________________

a) *Zile karama walizopokea tokea uumbaji: uzima wa milele, tabia ya utakatifu, maskani nzuri, utawala juu ya kila kitu, yalibadilishwa na kifo, dhambi, na nchi iliyojawa na miiba.*

b) *Kwa kufanya hivyi, mwanadamu alirithi maisha ya dhambi na kifo, ambayo yanaishia kwenye mauti ya milele na maangamizi ya mwisho.*

**7. Je, ni urithi gani tulioupata na hali ya sasa ya mwanadamu ni ipi? (Warumi 5:12).**

____________________________________________________________

**8. Je, kuna mtu ye yote mkamilifu ama mwenye haki kabisa katika ulimwengu huu? Je, ni matokeo gani ambayo kila mwanadamu ni lazima akutane nayo? (Warumi 3:10 – 12, 23; 6:23).**

a) *Hakuna mwenye* ____________________________________________

b) *Wote* ____________________________________________________

c) *Kwa maana mshahara wa dhambi ni* ________________________________

## *JE, KUNA NJIA YO YOTE YA KUTOKEA?*

**9. Je, Mungu anataka kwamba mwenye dhambi afanye nini? Ezekieli 33:11.**

____________________________________________________________

**10. Je, ni kwa njia ya nani pekee twaweza kuokolewa? Matendo 4:11, 12.**

____________________________________________________________

**11. Je, ni ufumbuzi gani ambao Mungu ameufanya? Yohana 10:7, 9.** __________________

**12. Je, Yesu anatutaka sisi tufanye nini? Mathayo 11:28, 29.**

____________________________________________________________

**13. Je, daraja pekee kati ya uzima na mauti ni lipi? Yohana 14:6.** ____________________

## *AHADI ZENYE KUTIA MOYO*

**14. Je, Mungu anawapatia nini wale ambao wanamwamini Yesu kabisa? 1 Yohana 5:11, 13.**

____________________________________________________________

**15. Je, kuna ye yote wa kukataliwa na Yesu ajapo Kwake ili kuokolewa? Yohana 6:37.**

____________________________________________________________

*Mungu anahitaji kutuhesabia haki sisi bure tu, yaani, kutangaza msamaha juu yetu na kutupatanisha sisi kwa neema Yake katika Kristo. ''Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu.'' (Warumi 3:24).*

## *HITIMISHO*

**16. Je, tunapasa kufanya nini ili kwamba tuitwe kuwa ni watoto wa Mungu na kupokea wokovu? Yohana 1:12.**________________________________________

*Kwa kumpokea Kristo, tunafikia kumfahamu pamoja na kuifahamu sheria Yake, kwamba Ndiye Bwana wetu. Tutamtii kwa njia ya upendo na kwa ajili ya kile alichotutendea sisi, nasi tutajitahidi kwa kila siku kuishi pamoja Naye. Kusudi la kifo Chake ilikuwa ni kutuokoa sisi kutoka katika bonde la magonjwa na maumivu, na kutupatia sisi urithi wa uzima wa milele. Hii ni habari njema. Ama wewe unaonaje?*

---

***Uamuzi wangu:*** *NInaamini ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa, nami ninaazimia kuichunguza kila siku.* ❏ *Ndio* ❏ *Hapana* ❏ *Nahitaji maelekezo zaidi*

---

# 4 HATUA NNE ZA KUIFIKIA AMANI YA NDANI NA FURAHA



Kila mwanadamu anahitaji amani halisi pamoja na furaha...

Je, yawezekana kuipata amani na furaha hii kutokana na mali, starehe, heshima, jinsia, madawa ya kulevya, ama pombe? K wa vyo vyote, hapana. Hizi ni njia potofu.

Msanii mmoja maarufu wa kike Marilyn Monroe alimweleza mwandishi mmoja wa habari: "Mimi nashangazwa na uzuri wangu, pesa ninayo, sipungukiwi na kitu. Lakini sijapata kuwa na furaha."

Lakini, je, amani na furaha inamaanisha kutopata matatizo? Twawezaje kuwa na amani na Mungu, dhamana ya msamaha Wake, tumaini thabiti na linalorudiwa, na uhakika ya kwamba iwapo tutakufa leo tutapata uzima wa milele?

## JE, UFUNGUO WA KUPATA AMANI NA FURAHA NI UPI?

**1. Jina la ufunguo huo ni lipi? Waebrania 11:6. ___________________________________**

**2. Imani sio:** *Kuchukulia jambo fulani ama kuwa na msimamo usio na uhakika. Kwa mfano,''Jua litachomoza kesho'' ama "Ninadhani kwamba jambo hili ama lile laweza tokea."*

- *Ni uthibitisho tu.* - *Hisia za muda mfupi tu.*
- *Ni kuongea tu juu ya dini.* - *Kulichukulia jambo fulani kama lilivyotolewa. Hii ni sehemu yake tu.*

**Imani ya kweli ni nini? Waebrania 11:1. ________________________________________**

- *Tumaini lisiloyumba juu ya ahadi za Mungu.*
- *Kuwa na imani juu ya Mungu na katika neno Lake.*
- *Kufahamu, kutumainia, na kujitoa kwa mtu fulani kwa kuchagua.*
- *Tunapasa kuwa na imani halisi katika Kristo, aliye Mtoaji wa uzima na Biblia.*

## HATUA NNE KATIKA UFAFANUZI WA IMANI (WAEBRANIA 4:16)

**3. Hatua ya kwanza: KUMFAHAMU YESU.**

**Kumfamu Yesu kunahusiana na kufanyeje? Yohana 17:3.**

_______________________________________________________________________

*Tunapasa kumfahamu yule tunayemwamini na ni nini tunachoamini.*

**4. Yesu ni nani?**

a) *Mwana wa Mungu wa milele. Mathayo 16:16.*
b) *Muumbaji. (Yohana 1:1-3, 14; Wakolosai 1:16)*
c) *Mtoaji wa Sheria.(Nehemia 9:13; 1 Wakorintho 10:4)*
d) *Mwokozi. (Luka 19:10)*
e) *Rafiki yetu. (Yohana 15:14, 15)*
f) *Mpatanishi. (1 Timotheo 2:5)*
g) *Bwana na Mfalme. (Ufunuo 17:14)*
h) *Hakimu. (Matendo 10:42)*

**5. Amefanya nini kwa ajili yangu?**

a) *Amefananishwa na wanadamu. (Wafilipi 2:7)*
b) *Aliishi pasipo kutenda dhambi. (Waebrania 4:15)*
c) *Aliuchukua ___________________________wangu. (Isaya 53:5,6.)*

d) *Alikufa badala yangu, kwa ajili ya ___________________________ zangu. (1 Wakorintho 15:3)*

e) *Alifufuka kutoka katika wafu. (1 Wakorintho 15:20).*

f) *Ananiombea mimi. (1 Timotheo 2:5)*

g) *Aliahidi kurudi na kunichukua mimi Kwake. (Yohana 14:3)*

**6. Hatua ya pili: KUMTUMAINIA YESU. Sifa Yake kuu ni ipi? Yohana 3:16. _____________**

*Kadiri niuonavyo upendo Wake, nitaufungua moyo wangu Kwake, nitamtumainia, nami nitamweleza mambo yote yanayonifadhaisha.*

**7. Hatua ya tatu: KUZIKIRI DHAMBI ZANGU. Je, upendo Wake na utuongoze sisi kufanya nini? Warumi 2:4. ____________________________________________________________**

**8. Je, tufanyeje na dhambi zetu? 1 Yohana 1:8, 9. (Zaburi 32:5) Isaya 55:6, 7.**

_____________________________________________________________________________

*Wala hatupasi kutoa kafara kubwa za kimwili, wala kwenda safari za hija ama kuweka nadhiri ili kusamehewa na Mungu. Yeye anautaka moyo wetu. Anataka tuziungame na kuziacha dhambi zetu. (Mithali 23:26).*

**9. Hatua ya nne: KUMKUBALI YESU KAMA BWANA NA MWOKOZI WETU. Ufunuo 3:20. Tofauti iko wapi kati ya kumkubali Yesu kama Mwokozi wetu na kumkubali kama Bwana wetu? Yohana 1:12.**

a) *Kama Mwokozi wangu, ni lazima niamini ______________________________ mahali pangu.*

b) *Kama Bwana, na Mtawala wangu, ni lazima nitii ________________________________ Zake.*

*Hebu na tuseme pamoja na Paulo, "Bwana, wataka nitende nini?"*

## *IMANI HALISI NA YA KITAMBO*

**10. Je, kuna tofauti gani kati ya imani halisi na imani ya kitambo?**

a) Imani halisi yapasa kujihusisha na ubinadamu wetu wote, maadamu sisi tu binadamu wenye sehemu tatu.

- HOJA (akili): Kumfahamu Yesu na kuamini ya kwamba Yupo.
- MOYO (hisia): Kumtumaini, kuufungua moyo wetu, na kuziungama dhambi zetu zote Kwake.
- HIARI (maamuzi): Kuhiari kumtii Yeye.

b) Imani halisi inamaanisha kujitoa kabisa Kwake.

c) Hatuhitaji kuwa wakamilifu ndipo tuje kwa Kristo. Hebu na twende Kwake kama tulivyo. (Yohana 6:37).

d) Tunahitaji kumruhusu aingie katika maisha yetu na kuishinda tabia yetu. Pale tabia yetu inapotawala, matamanio yetu yote hupinduka kuzunguka ndani yetu wenyewe. Pale Kristo awapo katika kiti cha moyo wetu, matamanio yetu yatakuwa yamekazwa kwa Mungu.

e) Tunapasa kufanya mapatano pamoja Naye, mapatano ya upendo, kama vile katika ndoa.



## *MATOKEO YAKE*

**11. Kwa njia ya Kristo tutakuwaje? 2 Wakorintho 5:17. ______________________________**

**12. Je, Mungu anatuahidi nini kuhusu dhambi zetu? Mika 7:18,19; Isaya 1:18.**

______________________________________________________________________________

*Tutafurahia wokovu, kwani yeye aliye Naye Mwana anao uzima.*

**13. Je, Yesu anampatia nini kila nafsi inayomkubali? Yohana 14:27.**

_________________________ *ya ndani. Tutapatanishwa na Mungu.*

## *HITIMISHO*

Mungu anataka kukufanya uwe na furaha leo!
Anataka kukusamehe dhambi zako na kukupatia wokovu.
Anataka kukuita kuwa ni mtoto Wake hivi leo.
Swali ni hili: Je, utamruhusu?
Je, umemkubali Yesu maishani mwako kama Mwokozi na Bwana?
Ulikiri hili kwa Mungu hivi sasa katika sala.

---

***Uamuzi wangu:*** *NInaamini ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa, nami ninaazimia kuichunguza kila siku.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

---

# 5 NAMNA YA KUBORESHA UTU WETU



Sisi sote tunataka kuwa na utu unaovutia. Wengi hushangaa: Je, ni kwa nini mimi niko jinsi hii? Nawezaje kuibadilisha hali hii? Kwani siku zote nilikuwa hivi? Je, naweza kuwa tofauti?

## HALI YA MWANADAMU KABLA NA BAADA YA DHAMBI

1. **Je, mwanadamu alikuwaje pale alipotoka mokononi mwa Muumba? Zaburi 8:5, 6. ______________________________**

2. **Dhambi aliharibu furaha ya mwanadamu. Ardhi nayo ilizalisha nini? Mwanzo 3:17, 18.**

   ______________________________________________________________________

   *Moyo wa mwanadamu ilipanda mbegu yenye sumu ya uovu: kiburi, wivu, kijicho, uasi.*

3. **Tabia ya mwanadamu ikawaje? Isaya 59:9-12.**________________________________

   *Utu wa mwanadamu ulivurugwa. Tabia yake iliharibiwa naye akatengwa kutoka kwa Mungu na akahukumiwa kifo. Isaya 59:2.*

4. **Je, haki ya mwanadamu imelinganishwa na nini? Isaya 64:6.**

   ______________________________________________________________________

   ***Kuwa mwenye haki humaanisha** kuafikiana na kipimo kilichotolewa na Mungu. Mwanadamu alikuwa katika maafikiano kamili pamoja na ile sheria ya Mungu. Lakini dhambi ndio iliyofanya kuwa isiwezekane kwake kufikia kile kiwango kinachotakiwa na ile sheria. Wazo chafu latosha kututenga sisi kutoka kwenye haki kamili.*

5. **Je, ni miujiza gani 4 ambayo Mungu anataka kuifanya katika maisha yetu? 1 Wakorintho 1:30.**

   *a) HEKIMA. Tunaitwa tuwe wenye haki.*
   *b) ____________________ Anatutaja sisi kama wenye haki.*
   *c) ____________________ Anatufanya kuwa wenye haki*
   *d) UKOMBOZI. Anatufanya sisi kuwa wa kudumu milele.*

6. **Muujiza wa kwanza una jambo gani? WITO WA MUNGU KWENYE HAKI.**

   *a) Anatuvuta sisi Kwake Mwenyewe. (Yohana 12:32).*
   *b) Anatuita. (Mathayo 11:28).*
   *c) Anatutafuta kama kondoo aliyepotea. (Mathayo 18:12, 13).*
   *d) Anatufanya tumwonee Mungu shauku. (Zaburi 63:1).*
   *e) Anatupatia sisi imani. (Yohana 6:29).*
   *f) Anatuonesha sisi dhambi zetu. (Yohana 16:8).*

7. **Je, mujiza wa pili unahusu nini? KUHESABIWA HAKI (KUTAMKWA KUWA MWENYE HAKI, HATA KAMA NI MWENYE HATIA)**

   *a) Kristo anatuhesabia sisi sifa Zake. Kufanyika mwili Kwake, maisha Yake yasiyo na dhambi, kafara na kufufuka Kwake kunakufanya kule kuhesabiwa haki kwetu kuwezekane. Kwa njia ya maisha Yake makamilifu na yasiyo na dhambi, aliyafikia madai ya ile sheria. Warumi 8:34. (Waebrania 2:14, 15). Kwa njia ya maisha Yake, Kristo alilipa lile deni ambalo sisi tulipasa kulilipa wenyewe kwa ajili ya kuasi kwetu. (Isaya 53:5, 6; Warumi 5:10).*

b) *Ni kukubali kwetu, kwa njia ya imani, juu ya tendo hili la Mungu kwa niaba yetu ndilo linalomfanya Mungu atutamke kuwa wenye haki. Huku ndio KUHESABIWA HAKI.*

**Matokeo yake ni nini? Warumi 5:1. ________________________________**

**8. Faida za haki ya kuhesabiwa ni zipi? (Kuruzukiwa, kupewa kama zawadi, kupewa bure).**

a) *Tunapewa ________________________________ Isaya 1:18; 43:25.*

b) *Yohana 1:12. Tunatamkwa kuwa ni ________________________. Warumi 8:16.*

c) *Luka 10:20. Majina yetu yameandikwa katika ________________________________*

d) *Jambo hili Yesu alilifafanua kwa ule mfano wa Farisayo na Mtoza Ushuru. Luka 18:9 – 14.*

**9. Mujiza wa tatu: KUREJEZWA KWA HALI ILIYOPOTEA. Je, mwanadamu aweza kuibadili tabia yake kwa jitihada zake mwenyewe? Yeremia 13:23; Warumi 7:24. ____________**

*Katika wakati ule ule Kristo anapotutangaza sisi kama wenye haki, Yeye anatenda mujiza mwingine ndani yetu kwa kututakasa kwa njia ya HAKI YAKE YA KUPEWA. Waefeso 4:24.*

**10. Je, Mungu anataka kufanyaje na akili pamoja na moyo wetu kwa njia ya neema Yake? Ezekieli 36:25-27. ________________________________**

a) *Badiliko hili la moyo linatuwezesha sisi kuitii ile sheria ya Mungu. Waebrania 10:16.*

b) *Kristo anapokaa moyoni mwetu, anautakasa kwa Roho Wake Mtakatifu na kutupatia sisi asili mpya. Wagalatia 2:20. (Wakolosai 3:5-10).*

**11. Je, ni sehemu gani za mwanadamu zinazotakaswa? 1 Wathesalonike 5:23.**

________________________________________________

a) ***ROHO** – mawazo* b) ***NAFSI** – hisia.* c) ***MWILI** – tabia za maisha.*

*Matendo mema ni matokeo ya kuhesabiwa haki, sio njia ya kuupatia. (Waefeso 2:10).*

**12. Je, ni lini ambapo mujiza wa nne wa UKOMBOZI ama KUTUKUZWA utakapofanyika? 1 Yohana 3:2. ________________________________**

*Tutafanana Naye na kubadilishwa kuwa katika kutokufa pale tutakapofufuliwa kutoka mautini. Tutakuwa na tabia kamilifu (Ufunuo 21:5). Kutakuwako na haki ya milele katika ile paradiso iliyorejezwa.*

**13. Je, nifanyeje ili kwambaYesu akaifanye miujiza hii maishani mwangu?**

a) *Itikia wito Wake. (Isaya 45:22).*

b) *Kumwamini na kumkubali Yeye kama Mwokozi na Bwana wangu. (Matendo 16:31).*

c) *Kuzitubia dhambi zangu. (Matendo 3:19).*

d) *Kuipokea Sheria Yake Takatifu. (Waebrania 5:8,9).*

e) *Kuyafanya upya maamuzi yangu kwa kila siku.*

f) *Kustahimili hata mwisho. (Mathayo 24:13).*

**14. Mpango wa Mungu kwa mwanadamu umefafanuliwa katika mfano wa mwana mpotevu. (Luka 15:11-24).**

Kisa cha mwana mpotevu huonesha ule mpango wa ukombozi kwa mwanadamu. Yule mwana anayekaa nyumbani humwakilisha Adamu katika Edeni. Anapoondoka nyumbani, anaanguka. Mwana mpotevu alitumia vyote alivyokuwa navyo, jambo ambalo linaashiria kutwezwa kwa maadili. Utumwa huu ni utumwa wa Shetani. Alipozingatia moyoni; hii ni kazi ya kimya kimya ya Roho Mtakatifu. Analitambua kosa lake pale anaposema, “Nitaondoka, niende kwa baba yangu.” Kuambatana na baba yake ni kule kuhesabiwa haki. Lile vazi bora la baba ni ile haki ya kuhesabiwa. Kuvikwa upya kwa vazi lile ni haki ya kupewa. Hatimaye, ile karamu inawakilisha kutukuzwa.

## 15. Je, ni furaha zipi tatu ambazo Mkristo huzipata katika Yesu?

*Moyo wetu umejaa furaha tunapopata habari hizi njema.*

a) Kwanza tunapata **furaha ya wokovu**. (Zaburi 51:12).

b) Kisha **furaha ya utii**. (Zaburi 119:174).

c) **Furaha ya milele**. (Isaya 25:10).

---

***Uamuzi wangu:*** *Ninaamini ya kwamba nimehesabiwa haki kabisa kwa imani na kwamba matendo ni matunda yake na uthibitisho wa upendo wangu.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

---

# 6 UFUMBUZI BORA ZAIDI JUU YA MATATIZO YANGU NA YANAYONIHUSU



Kila mwanadamu hukabiliana na fadhaa na matatizo! Haya yaweza kuhusisha familia, kazi, afya, mambo ya kijamii ama ya kibinafsi na maisha ya kiroho.

Kwa mtoto mgonjwa awapo katika kitanda cha mauti na mama yake akiwa katika kukata tamaa. Mume wake ni mlevi, ambapo mwanaye anaugua kutokana na kukosa chakula, mavazi, na wana shida ya makazi maridhawa. Hawa wanahitaji badiliko.

Tutafanyaje pale tuwapo na matatizo juu ya afya, kazi, familia yetu, ama mambo ya ustawi wangu? Pengine unajisikia majuto kutokana na mapungufu yako ama pengine unajisikia kufadhaika, upweke, na kukata tamaa usifahamu kama ni kwa nani ambako utaufungua moyo wako kwake.

Sala ndio ufumbuzi bora zaidi. Yaweza kulinganishwa na kumpigia Mungu simu moja kwa moja. Zaburi 34:6.

**1. Twaweza kuyafafanuaje maombi?**

- *"Maombi ni muhimu; kwani ndio uhai wa nafsi."*
- *"Maombi ni kuufungua huu moyo kwa Mungu kama kwa rafiki."*
- *"Maombi ni ufunguo mkononi mwa imani ili kuzifungua hazina za mbinguni kulikotunzwa mali nyingi mno za enzi kuu." Ellen G. White, Steps to Christ, uk. 94.*
- *"Ni vitamini za kiroho."*

**2. Je, ni njia gani za mawasiliano ambazo Mungu alizitoa baada ya lile anguko?**

*Rafiki yetu Yesu anataka kutusaidia sisi, **Naye anaongea nasi kupitia Neno Lake**. Tulitafakari kwa kila siku. (Yohana 15:15) (Matendo 17:11). – Tunaongea Naye kwa njia ya maombi. (Danieli 9:20).*

## *LINI, WAPI NA TUOMBEJE?*

**3. Wale wanafunzi walimwomba Yesu kufanya nini? Luka 11:1.**

__________________________________________________________

**4. Ni aina zipi za maombi tulizo nazo?**

*a) **Ya wote**. Mtu mmoja huomba na kusanyiko lote husikiliza kwa kicho. Ombi hili lapasa kuwa fupi.*
*b) **Familia**. Kila asubuhi na kila jioni, familia inapasa kusoma Neno la Mungu na kuomba.*
*c) **Kabla ya chakula**. Tunapasa kumshukuru Bwana kwa ajili ya chakula alichotujalia na kumwomba akibariki.*
*d) **Faragha**. Mathayo 6:6. "… Ni mawasiliano ya siri na Mungu ambayo huuimarisha uhai wa nafsi." Ellen G. White, Education, uk. 254.*

**5. Tuombe lini?**

*a) Twaweza kuomba **tunaposafiri ama tunapofanya kazi**. Twaweza kuomba kwa kimya kimya. (1 Wakorintho 14:15).*
*b) **Panapo nyakati za hatari ama uhitaji.** (Yona 2:1).*
*c) Vizuri iwapo tungeomba mara tatu kwa siku (Danieli 6:10). **Daima tuwe katika roho ya maombi**. (1 Wathesalonike 5:17).*

**6. Tuepuke nini tuombapo? Mathayo 6:7, 8.** ______________________________

*Tuombe kwa maneno machache na dhahiri, kwa unyofu. Ile sala ya Bwana ni mfano bora juu ya namna ambavyo sala ingepasa kuwa.*

7. **Tuwaombee nani?**

   a) ***Wagonjwa, na watu mbali mbali****. (Yakobo 5:13-16).*
   b) ***Wajumbe wa Mungu pamoja na ustawi wa Injili****. (Matendo 12:5; Habakuki 3:2).*
   c) ***Kumwagwa kwa Roho Mtakatifu****. (Luka 11:13).*
      *Kielelezo cha sala: 1. Mweleze Baba: Baba yetu   2. Umshukuru: Asante kwa ajili ya …*
      *3. Ombea: mahitaji yetu, kwa ajili ya wengine, kuombea msamaha wa dhambi4. Katika jina la Yesu.*
   d) *Hitimisho: "Amin" ikimaanisha "Na iwe hivyo."*

## *ILI KWAMBA MUNGU ATUSIKILIZE, TUNAPASA KUWEJE?*

8. **Tunapasa kuonyesha nini? Mathayo 6:5.** *Unyofu, sio kufuatisha* ____________________

9. **Tuombeje? Yakobo 1:6, 7.** ____________________________________________

   *Imani inalinganishwa na mbegu ambayo inahitaji kupandwa, kumwagiliwa na kutunzwa. Ni lazima ilishwe kwa kujifunza Neno la Mungu kila siku. (Warumi 10:17).*

10. **Tunapasa kujinyenyekeza. Je, ni mfano gani unaotufundisha jambo hili? Luka 18:9-14.**

    ____________________________________________________________

11. **Kwa sala ya kicho, tuombeje? Warumi 14:11.** ______________________________

    *Waweza pia kuomba ukiwa umesimama, mara zote ukiwa umeinamisha kichwa, ukifumba macho na mikono yako.*

12. **Mara zote tunapasa kuwa na roho ya jinsi gani? Mathayo 6:25.** *Roho ya* ____________

    *Hili limeoneshwa katika ule mfano wa wadaiwa wawili. (Mathayo 18:23-35).*

13. **Je, ni neno gani tupasalo kulisema kila mara tumwombapo Mungu kitu cho chote? Mathayo 26:39.**____________________________________________

    *Mungu ayajua mahitaji yetu. (Warumi 8:26). Tumruhusu Mungu atufinyange, kama vile mfinyanzi anavyoufinyanga udongo kwa mikono yake. (Yeremia 18:6). Mungu aweza kutoa jibu. Kama bado, SUBIRI. Yeye anajua lililo bora kwetu.*

14. **Na tuwe wastahimilivu. Je, ni nani aliyekuwa mfano katika ustahimilivu katika Luka 18:1-7?**

    ____________________________________________________________

15. **Je, tuzingatie nini ili tuweze kusikizwa na Mungu? 1 Yohana 3:22. (Mithali 28:9).**

    ____________________________________________________________

16. **Tuombe kwa jina lipi? Kwa nini? Yohana 16:23, 24.**

    ____________________________________________________________

    *Dhambi ndio inayotutenga sisi na Mungu. Ni kwa njia ya neema ya Kristo pekee ndipo twaweza kutarajia maombi yetu kukifikia kiti cha enzi cha Mungu.*

## *FARAJA NA FURAHA KATIKA MAOMBI, MITHALI 15:8, 9.*

17. **Tunapojiona kuzidiwa na matatizo, ni nani ambaye twaweza kumwita atusaidie? Mathayo 11:28.** ____________________________________________

18. **Mungu anatusihi tufanyeje? Warumi 12:11, 12.** *Tuwe* ______________________________

    *Hebu na tuitumie "simu" ya Mungu, ufunguo ulio katika mkono wa imani, vitamini ya nafsi:*

- *Kumsifu, kumshukuru, kuziungama dhambi zetu Kwake, kumweleza fadhaa zetu, na kuendelea siku kwa siku kudumisha mahusiano binafsi pamoja Naye.*
- *Kuendeleza mazowea ya kuomba katika familia yako na kuwafundisha watoto wako namna ya kuomba.*
- *Hii ndio njia pekee tuwezayo kuishi katika furaha na katika amani, tukijiona kuwa na uhakika ya kwamba matatizo yetu makubwa yatashughulikiwa na kwamba Yeye atatutegemeza.*

***Uamuzi wangu:*** *Nataka niwe ninasali kwa kila siku, kwani maombi ndio uhai wa nafsi na ndio njia ya kuwasiliana pamoja na Mungu.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

# 7 JE, NI NANI ATAKAYEITAWALA DUNIA HATIMAYE?



Pengine itakuwa ni Marekani, Urusi, Uchina, Japani ama taifa jingine lenye nguvu? Hitla pamoja na Napoleoni walikuwa na ndoto ya kuwa dola kubwa zaidi, lakini: Maneno manne yaliyoandikwa zaidi ya miaka 2,600 iliyopita yaliwazuwia wasiwe hivyo!

**1. Je, ni wapi pekee tuwezapo kupata nuru kuhusu siku zijazo? 2 Petro 1:19.**

_______________________________________________

Ni Mungu pekee anayezijua siku zijazo. (Isaya 46:9,10).

## *UFUNUO WA AJABU JUU YA SIKU ZIJAZO: DANIELI SURA YA 2*

Nebukadneza, Mfalme wa Babeli, aliyepata kuishi kiasi cha miaka 600 Kabla ya Kristo aliota ndoto, lakini akaisahau. (Danieli 2:1). Akawaamuru wachawi na wasihiri wake ya kwamba na wamwoneshe yeye ile ndoto pamoja na tafasiri yake, lakini wao hawakuweza kufanya hilo. (Mstari wa 3). Mfalme akasaini tamko ambalo liliamuru ya kwamba wenye hekima wote wa Babeli ambao miongoni mwao alikuwamo Danieli pamoja na rafiki zake, wauawe. (Mstari wa 14). Danieli akamwomba Mfalme ampatie muda kidogo, yeye pamoja n a rafiki zake walimwomba Mungu, Naye Mungu akamwonesha Danieli kila jambo. (Mistari ya 15 -19).

**2. Je, ni nani pekee awezaye kuelekeza na kuifunua hatima ya mataifa? Danieli 2:20-22, 27, 28.**

_______________________________________________

Danieli hata alimwonesha yule mfalme yale aliyokuwa akiyawaza moyoni pale alipokuwa amelala. (Mistari ya 29, 30).

**3. Nebukadneza aliona nini katika ndoto yake? Danieli 2:31-35.**

*Aliona ____________________ kubwa sana. Kichwa chake kilikuwa cha ____________________; kifua na mikono yake ya __________________; tumbo lake la __________________; na miguu yake ya ____________________ na ____________________.*

## *MAANA YA ILE NDOTO*

**4. Ni ufalme gani uliowakilishwa na kile kichwa cha dhahabu? Danieli 2:37 – 38.**

_______________________________________________

- *Ufalme huu ulikuwa ni wenye fahari kubwa. Jiji la Babeli lilikuwa na mitaa iliyopewa pambizo za miti pande zote pamoja na majumba ya kifalme yenye kupendeza sana. Bustani zake zenye kuning'inia zilikuwa ni mojawapo ya maajabu saba ya dunia ile ya kale. Kiasi kikubwa cha udongo kiliwekwa katika tabaka zilizoinuliwa na hivyo miti mikubwa iliota humo.*
- *Dhahabu ilikuwako kwa wingi. Katika lile hekalu kuu la Marduk kulikuwako na sanamu ya Beli na meza kubwa sana ya mita 12 x 4.5, hivyo vyote vikiwa vimetengenezwa kwa dhahabu safi yenye uzito wa kg. 23,000. Kulikuwako pia simba pamoja na sanamu vilivyotengenezwa kwa madini hiyo hiyo, ambavyo ilikuwa na kimo cha mita 5.4.*
- *Jiji lile lilionekana kuwa ni lisiloshindika kwa vita. Kulingana na Herodotus, mwanahistoria Mgriki,*

*lilizungukwa na ukuta wenye kimo cha mita 60 juu na handaki la maji lenye kina kirefu.*

- *Lilikuwa na akiba ya chakula kwa miaka ipatayo 20. Jiji lilikuwa na maji kwa wingi maadamu Mto Frati ulitiririka chini ya kuta zake, hata katikati ya jiji.*

**5. Kifua na mikono ya fedha ikiwakilisha UMEDI-UAJEMI (538 – 331 Kabla ya Kristo). Ufalme ule ungelinganishwaje na ule uliotangulia? Mstari wa 39. ________________**

- *Ile mikono miwili iliwakilisha zile sehemu mbili zilizounda ufalme ule: Umedi na Uajemi.*
- *Kwa mara ya kwanza, sarafu za fedha zilitumika katika miamala ya kibiashara.*

**6. Je, unabii ulisema nini juu ya ufalme huu uliowakilishwa na tumbo la shaba? Mstari 39.**
*Sehemu hii ya sanamu iliwakilisha UYUNANI (331 – 168 K.K.)*

- *Silaha zilizotumiwa na Wagriki zilitengenezwa kwa shaba nyeusi. Askari wa Kigriki waliitwa kuwa ni "askari wa shaba."*
- *Tumbo: Alexanda Mkuu alikuwa ni mtumwa wa tumbo lake, alikufa akiwa kijana kabisa kutokana na tafrija alizozishiriki. Alexanda alikufa akiwa na umri wa miaka 32, akiwa anakunywa mzunguko wa pili wa kinywaji chenye nguvu sana, kilichokuwa ni kiasi cha lita 5 za divai. Ufalme wake hatimaye ulipasukana.*
- *Ule mng'ao wa muda wa ile shaba nyeusi ulielekea kuonyesha kuondoka kwa ule utukufu wa ufalme wake.*

**7. Ule ufalme wa nne, uliofananishwa na ile miguu ya chuma, ungekuwaje? Mstari 40.**

________________________________

*DOLA YA RUMI (163 K.K. – 476 B.K.)*

- *Dola ya Rumi ilidumu kwa miaka 644. Ulikuwa ni utawala wenye kuparuza na baridi, kama vile kilivyo chuma. Ulikuwa ni wenye ukatili na kutisha, na jambo hili laweza kuonekana katika lile jambo baya mno lililofanywa na Nero pamoja na wafalme wengine.*
- *Silaha zilizotumiwa na Warumi zilikuwa ni panga fupi za chuma.*

**8. Je, ni ufalme gani huu uliowakilishwa na ile miguu ya chuma kilichochanganyika na udongo wa mfinyanzi? Mistari 41 – 43. ________________________________**

- *Kati ya karne ya nne na ya tano Dola ya Rumi iligawanyika katika sehemu 10. Ilidhoofika chini ya shinikizo la makabila ya Kijerumani yaliyokuja tokea kaskazini mwa Ulaya. Hatimaye, eneo lile la Dola ya Rumi likakaliwa na Wafranka (Ufaransa), Wajerumani Ujerumani, Wa-Anglo-Saksoni (Uingereza), Walombadi (Utaliano), Wasuevi (Ureno), Wavisigothi (Uhispania) na Waburgandia (Uswisi). Waheruli, Wavandali na Waostrogothi hivi sasa hawako. Mataifa haya yote yalikuwa kwa sehemu ni yenye nguvu na kwa sehemu ni dhaifu.*
- *Wangethubutu kujiungamanisha upya kwa njia ya kuoleana kimataifa.*
- *Justiniani, Mfalme wa Mashariki, Charles V; Filipo II; Louisi XIV; Napoleoni; Wilhelm II; na Hitla walijaribu kuufikia umoja huu kwa kutumia nguvu ili kuifikia ndoto yao ya kuunda ufalme ulio mkubwa, lakini walishindwa.*

**9. Je, ni maneno gani sita yaliyoandikwa katika Biblia ambayo yanatuambia ya kwamba juhudi zote za kuiunganisha Ulaya zingefeli? Mstari 43.**

________________________________________________

**10. Je, Mungu atasimamisha kitu gani pale mataifa haya yanapojaribu kuungana? Mistari 34, 44, 45. ________________________________________**

*Maneno haya, "bila kazi ya mikono" humaanisha ya kwamba silo tukio la kibinadamu bali la kimbingu.*

**11. Je, jiwe lile lililoipiga ile sanamu lilimwakilisha nani? Matendo 4:11; 1 Wakorintho 10:4.**

____________________________________________________________

## *HITIMISHO*

**12. Je, ni nani atakayekuwa mtawala wa utawala wa dunia ujao? Ufunuo 11:15.**

____________________________________________________________

**13. Sasa basi ya kwamba tukio hili la kipekee li karibu sana kutokea, ni wito gani ambao Bwana anautoa? Luka 12:40.**

____________________________________________________________

***Uamuzi wangu:*** *Nataka niwe ninasali kwa kila siku, kwani maombi ndio uhai wa nafsi na ndio njia ya kuwasiliana pamoja na Mungu.* ❏ *Ndio* ❏ *Hapana* ❏ *Nahitaji maelekezo zaidi*



# 8 CHIMBUKO LA MASHAKA HAYA YA ULIMWENGU YALIYOPO

Kuna mashaka katika kila sekta ya jamii, na kila taifa hivi sasa linakutana na mageuzi. Kulikuwako na vita kule Mashariki ya Kati, mapambano katika Amerika ya Kati, misukosuko katika Afrika, kukosekana kwa usalama mitaani, wizi, ghasia, hatia za watoto wadogo, n.k. Kuna mashaka pia katika kupanda kwa gharama za kifedha ulimwenguni, kupanda kwa gharama za maisha, taabu, njaa, na migomo. Madeni ya fedha za kigeni yanatishia uchumi wa nchi za Ulimwengu wa Tatu.

Katika mambo ya asili, huko nako tunaona mashaka – matetemeko ya nchi, mafuriko, ukame, pamoja na vimbunga, kuganda kwa barafu katika maeneo makubwa, pamoja na mawimbi ya ghafla ya joto kali kurudiwa kila mara. Familia mbali mbali pia zinayapitia mashaka. Katika Marekani, kuna talaka zipatazo 6,500 kwa kila siku, ambazo ni zaidi ya milioni moja kwa mwaka. Kati ya wanawake wa umri wa miaka 30 na 40, sita katika kumi wamezipitia talaka, ambazo ni kiasi cha 60%. Katika Ufaransa, moja katika ndoa mbili huishia talaka.

Afya ya ulimwengu imetishiwa. Idadi ya wagonjwa wa Ukimwi inapanda juu kwa kasi, na mara wahanga wake watafikia idadi ya milioni 18. Haya yote huonyesha ya kwamba kuna kitu kinafanyika, lakini ni nini?

**1. Kutokana na hali hizi, watu wanasumbuka na nini? Luka 21:25, 26.** ____________________

*Je, ni kwa nini haya yote yanatokea jinsi hii? Matukio haya yote, mabadiliko, na mashaka haya yanatangaza nini?*

**2. Je, wanafunzi walimuliza nini Yesu? Mathayo 24:3.**

______________________________________________________________________

## *DALILI ZA ULE MWISHO*

Hata kama hakuna mtu ajuaye kwa usahihi siku na wakati wa kuja kwa Yesu (Mathayo 24:36), kutakuwako na hali fulani ambazo ni ishara zinazoelekeza kwenye ule wakati wa kuja Kwake. Shida ambayo tumepata kuitaja hapa ni moja wapo ya ishara ya siku za mwisho.

**3. Kutatokea nini miongoni mwa mataifa? Mathayo 24:6, 7.** ______________________________

*Kumekuwako na vita mara nyingi, lakini vita hizi za dunia ni pato la karne yetu hii. Kuna ushindani mkubwa wa nguvu za silaha za vita. Mataifa madogo yanatokea kuwa na nguvu (Yoeli 3:10). Silaha za nuklia zilizoko siku hizi, zinaweza kuiangamiza sayari yetu hii kwa mara 50, bila ya kuzitaja silaha za kikemikali.*

**4. Licha ya haya yote, ni mikataba gani itakayosainiwa? 1 Wathesalonike 5:3; (Yeremia 6:14).**

______________________________________________________________________

**5. Hali ya kiafya ya watu, wanyama, na mambo ya asili itakuwaje? Mathayo 24:7.**

______________________________________________________________________

*Mwanadamu wa leo anaendelea kuwa mgonjwa kabisa, kansa, ukimwi, na mstuko wa moyo ni tauni yetu. Wanyama wanafugwa kinyume na asili, mboga zinatiwa viwatilifu na mbolea za kemikali kwa ajili ya kuzalishwa kwa wingi.*

**6. Je, Biblia inasema nini juu ya uharibifu wa mazingira? Isaya 24:4, 5, 7.**

______________________________________________________________________

**7. Je, mamilioni ya watu watasumbuliwa na nini? Mathayo 24:7.**

_______________________________________________________________

*Ripoti za Umoja wa Mataifa zinasema ya kwamba theluthi mbili ya wanadamu wanasumbuliwa na utapiamlo, na kila mwaka watoto million 12 hufariki kabla ya kuufikia mwaka wa kwanza wa maisha yao. Deni la fedha za kigeni katika nchi za Ulimwengu wa Tatu linalifanya tatizo hili kuwa gumu zaidi, kupanda kwa bei ya bidhaa hutishia kuharibu uchumi wa nchi nyingi.*

**8. Dalili nyingine ni zipi? Luka 21:11.** _______________________________

*Kwa kulingana na takwimu, kumekuwako na matetemeko ya nchi yapatayo 127,000 katika karne hii, ambazo ni mara 8,500 zaidi kuliko ilivyokuwa katika karne ya kwanza, na mara 31 zaidi kuliko karne zote zilizotangulia. Idadi ya vifo vinavyotokana na matetemeko ya ardhi imeongezeka mara 10 zaidi katika karne hii kuliko katika zile zilizotangulia.*

**9. Kutatokea nini katika sayansi katika siku za mwisho? Danieli 12:4.**

_______________________________________________________________

*80% ya mavumbuzi yote yamefanyika katika karne za mwisho zilizopita, na 90% yake ni za wanasayansi ambao wapo hai bado. "Wengi wataenda mbio huko na huko …" unakiangazia kipindi cha shughuli nyingi za kimaisha za wakati wetu pamoja na kasi ambayo mwanadamu anaweza kwenda na kurudi kutoka mahali pamoja hadi pengine.*

**10. Je, ni matatizo gani yatakayoibuka katika ulimwengu wa kazi? Yakobo 5:1-5.**

_______________________________________________________________

**11. Kupenda anasa, ngono, vurugu na rushwa zitafanana na wakati upi? Luka 17:26-30. Mwanzo 6:11).** _______________________________

*Uchu umekuwa ni mungu kwa wengi. Uzinzi, talaka, ubakaji, na vurugu ndizo zinatawala katika skrini za runinga na katika maisha halisi.*

*Dhambi za Sodoma (kujamiiana kwa watu wa jinsia moja) zimeongezeka kwa namna ya kutisha na ukimwi kwa vyo vyote ni matokeo yake. Mauaji yameongezeka kwa 900% katika miaka 10 iliyopita.*

**12. Je, kuna ishara zipi katika ulimwengu wa kijamii? 2 Timotheo 3:1-4.**

_______________________________________________________________

*Kutakuwako na kukosekana kwa ______________________ (Mathayo 24:12).*

**13. Je, ni dalili gani zitakazodhihirika katika ulimwengu wa kidini?**

*2 Timotheo 3:5. Mfano wa ______________________________*

*2 Timotheo 4:3, 4. Mafundisho ya uongo.*

*Mathayo 24:5, 11, 24. ______________________________ wa uongo.*

*Luka 18:8. Kukosekana kwa ______________________________*

*2 Petro 3:3, 4. ______________________________*

*Mathayo 24:14. Injili ______________________________*

## *HITIMISHO*

**14. Dalili hizi zote zinamaanisha nini? Luka 21:28-31.**

_______________________________________________________________

**15. Je, Mungu anatusihi sisi tufanye nini katika wakati huu makini? Luka 21:34-36.**

________________________________________________________________

Yakitokana na haya yaliyooneshwa hapo juu pamoja na utimilizo wa nabii mbali mbali za kibiblia ambazo zaendelea kutimilika mbele ya macho yetu, je, unaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho wa historia ya mwanadamu? Je, unapenda kujiandaa kukutana na Yesu ajapo mara ya pili?

***Uamuzi wangu:*** *Ninaamini ya kwamba dalili za nyakati zinautangaza ule mwisho wa ulimwengu, nami nahitaji kuwa tayari pale Kristo anaporudi.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

# 9 TUKIO KUBWA ZAIDI LA MILENIA YA TATU



Ulimwengu unaishi katika kutazamia matukio ya millenia mpya. Kuta kuharibika kwa ubinadamu ama ni mwanzo wa zama mpya?

Je, tutakufa kwa kuangamizwa na njaa, uchafuzi, gharika ya ulimwengu, ama kama tutafurahia ustawi mwema zaidi katika ulimwengu uliopangiliwa sana katika teknolojia yake mpya iliyoundwa na mwanadamu?

Ghasia zitafikia upeo wake katika ulimwengu wa vita za nuklia? Ama kama kipindi cha amani na maelewano kati ya mataifa kipo mbele yetu? Je ni kitu gani kinawangojea watoto wetu? Karne hii ya 21 italeta nini?

Sayansi ya anga za juu imefaulu kukamilisha mambo makuu. Mwanadamu ameweza kutua katika mwezi, kuishi katika kituo cha anga za juu, kuweka setelaiti mbali mbali katika anga na kupeleka mitambo ya kuchunguza katika sayari zilizo mbali, lakini hajajiandaa kwa ajili ya vita kubwa zaidi katika anga, vita ambayo haijapata kufikiriwa ama kwa ajili ya safari za kushangaza ya kuziendea nyota. Biblia inasema nini juu ya hili?

Dunia haitamalizwa na vita za kinuklia. Yesu Kristo ataingilia kati ya masuala ya wanadamu katika ule ujio Wake wa pili.

Tokea lile anguko la mwanadamu, maumivu, magonjwa, na kifo vikaingia, pamoja na ile ahadi ya kuja kwa Mwokozi. Mwokozi huyu alitazamiwa katika miaka 4,000 iliyopita. Ujumbe Wake ulikuwa: "ANAKUJA."

Nabii 333 za kibiblia zinaelezea juu ya kuja Kwake mara ya kwanza kwa kina, nazo zote zilitimilika kimahesabu kabisa.

## *TUMAINI LA KIMILENIA*

**1. Yesu Kristo Mwenyewe aliahidi nini? Yohana 14:1-3.** ______________________________

*Ahora el anuncio es: "ÉL REGRESA".*

**2. Je, ujumbe huu ulidhaniwaje na mamilioni ya Wakristo katika karne hizo zote? Tito 2:13.**

______________________________________________________________________________

**3. Ni kwa nini Yesu atarudi?**

a) Waebrania 9:28. Kwa __________________________________________________

b) Isaya 35:4-6. Ili ________________________________________mateso ya wanadamu.

c) Wafilipi 3:20-21. Kutupatia sisi ________________________ wa nchi iliyo nzuri zaidi.

d) Zaburi 96:13. Ili ___________________________________________

e) 2 Wathesalonike 1:7 -9. Ili kuwaangamiza ____________________________________.

## *JE, YESU ATAKUJAJE?*

**4. Je, Yesu atakuja namna gani? Matendo 1:9-11.**

______________________________________________________________________________

**5. Je, Yesu aliyefufuka aliweza kuonekana na kugusika? Luka 24:36-40.**

______________________________________________________________________________

**6. Pia atakuja kwa namna gani? Mathayo 24:30. ________________________________**

**7. Je, ni wanagapi watakaomwona? Ufunuo 1:7 (Mathayo 24:26, 27)**

________________________________________________________________________

**8. Ni nani watakaomsindikiza Yesu? Mathayo 25:31. ______________________________**

**9. Je, ni sisi pekee tutakaomwona? 1 Wathesalonike 4:15-16. ______________________**

## *KUTATOKEA NINI PALE ATAKAPOKUJA?*

**10. Je, kutatokea nini kwa wale waliokufa wakimwamini Kristo? 1 Wathesalonike 4:15, 16.**

*Tumaini lenye utukufu! Kukutana tena na wapendwa ambao kifo kiliwanyofoa kutoka kwetu! Kina mama ambao wamekuwa waaminifu watawapokea wale watoto waliokufa utotoni mwao. Jambo la kupendeza jinsi gani!*

**11. Je, kutatokea nini juu ya miili yetu yenye magonjwa na kukabiliwa na kifo? 1 Wakorintho 15:51-53.**

________________________________________________________________________

**12. Je, wale waovu watasema nini pale Kristo ajapo? Ufunuo 6:15, 16.**

________________________________________________________________________

*Watazikumbuka zile fursa zilizopotezwa na kule kuukataa kwao wito wa Mungu, lakini itakuwa wamechelewa sana. Watapotea milele.*

**13. Je, wale wenye haki watasemaje, nao watajisikiaje? Isaya 25:9.**

________________________________________________________________________

**14. Je, ile siku ya Bwana itakuja kwa jinsi gani? 2 Petro 3:10.**

________________________________________________________________________

**15. Naye anatupatia ushauri gani? Mathayo 24:42, 44.**

________________________________________________________________________

## *HITIMISHO*

Baada ya masomo haya mawili juu wakati wetu huu na kurudi kwa mara ya pili kwa Kristo, je, unadhani kwamba kuja Kwake ni karibu hasa, ama pengine bado una mashaka?

*__Uamuzi wangu:__ Ninaamini ya kwamba Yesu Kristo atarudi hivi karibuni kabisa, katika namna ya kuonekana na kupapasika.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

# SOMO LA 1 – 9

## *MASWALI YA KUTAFAKARI*

Kusudi la orodha hii ya maswali ni kuupima uelewa wako juu yale yaliyomo katika masomo haya uliyoyamaliza. Iwapo unapenda, unaweza ukayafanya mbele ya mkufunzi wako na kisha uyafuatilie yale maswali uliyojibu kwa usahihi. Iwapo una shaka lo lote, jaribu kuyapitia tena masomo haya na kumwuliza mkufunzi huyo.

**1) Neno "Biblia" linamaanisha nini?**

a. Mkusanyiko wa karatasi za zamani.
b. Mkusanyiko wa vitabu.
c. Kitabu Kitakatifu.

**2) Taja matabirio 2 tu kati ya 333 juu ya Yesu Kristo.**

*a.* ____________________________________________

*b.* ____________________________________________

**3) Yesu alisema: "Mimi ndimi ________________, na ____________________________ na _________________________."**

**4) Je, tunabadilika na kuwaje pale tunapompokea Yesu kama Mwokozi wetu?**

____________________________________________

**5) Tunahesabiwa haki (kusamehewa) na Mungu kwa njia ya:**

a. Imani
b. Matendo yetu
c. Dini

**6) Je, ni vipengee vipi vya mwanadamu ambavyo hutakaswa?**

a. ___________________________

b. ___________________________

c. ___________________________

**7) Hebu fafanua maana ya sala.**

____________________________________________

**8) Kwani tuombeje?**

____________________________________________

**9) Je, tunafaidikaje kutokana na kusoma Biblia?**

______________________________________________

**10) Je, ni funguo zipi 5 ili kuielewa Biblia?**

a. ____________________

b. ____________________

c. ____________________

d. ____________________

e. ____________________

**11) Je, ni nani anayewakilishwa na lile jiwe lililoivunja ile sanamu aliyoiota Nebukadneza?**

______________________________________________

**12) Hebu orodhesha dalili 2 za nyakati.**

a. ________________________

b. ________________________

**13) Je, ahadi ya Yesu kabla hajapaa kwenda mbinguni ilikuwa ni ipi?**

______________________________________________

**14) Je, ni kwa nini Yesu atarudi?**

______________________________________________

**15) Je, Yesu atakujaje?**

______________________________________________

**16) Kutatokea nini pale Yesu ajapo?**

______________________________________________

***Mada za Ngazi ya 2:*** *Siri ya lile Sanduku la Dhahabu la Agano, Njia Bora Zaidi ya Kuushinda Msongo, Je, Kuna Maisha baada Kifo? Mada hizi na nyinginezo zitakushangaza kwa usahihi wa Biblia katika majibu ya maswali ambayo wengi huuliza. Huwezi kuzikosa!*



# Anwani za Mawasiliano

## NORTH AND CENTRAL AMERICA

**Belize**: Email: info@labibliatienerazon.org
**Canada**: www.4truth.ca / Email: mail@4truth.ca
**Jamaica**: Tel.: (+1) 876-489 1658
imssdajamaica@gmail.com
**Puerto Rico**: Tel./Fax: (+1) 787-726-6192
Email: info@labibliatienerazon.org
**USA**: Email: info@sda1888.org
Web: www.sda1888.org
**Other Caribbean Islands**:
info@labibliatienerazon.org

## EUROPE

**Germany:** Tel.: (+49) 5406-8989952
geschaeftsstelle@reform-adventisten.net
**Italy:** Tel.: (+390) 861-781 110
missionicristiane@virgilio.it
**Spain:** Tel.: (+34) 96-151 2844
info@asdimores.org/asdimores@gmail.com
**The Netherlands:** Tel.: (+31) 313-416 222
Rehoboth@ZDAreformatie.org
**United Kingdom:** Tel.: (+44) 7766322052
treasury.bf@hotmail.com

## AFRICA

**Botswana:** imstso1844@gmail.com
**Cameroon:** Cel. & WhatsApp: (+237) 6 5315 6974
imscameroon1994@gmail.com
**Gambia:** imsgambia1914@gmail.com
**Kenya:** Cel.: (+254) 727-928-488
imskenyaunion@gmail.com
**Lesotho:** AfricanDivision@sda1844.org
**Liberia:** Tel.: (+231) 6-530 668
imssdarmlib2009@yahoo.com
**Malawi:** Cel.: (+265) 884 514 363
malawiunion@hotmail.com
**Nigeria:** Tel.: (+234) 803-744-7190
imsnigeriafield@gmail.com
**Rwanda:** Cel.: (+250) 788 660 278
rwanda_field@yahoo.com
**Seychelles:** imsseychelles1888@gmail.com
**Sierra Leone:** inter.miss.sl@gmail.com
**Sudan:** imssdarmssudanfield@yahoo.com
**South Africa:** Tel.: (+27) 76-615-9434
imssouthafricaunion@gmail.com
**Tanzania:** Tel.: (+255) 565 533 298
unoftzimssdarm@yahoo.com
**Uganda:** Cel.: (+256) 772 370 673
uimssda1844@yahoo.com
**Zambia:** Tel.: (+260) 211-282-805
zamunion@gmail.com
**Zimbabwe:** Cel.: (+263) 712 775 775
imssdazimfd@yahoo.com

## ASIA

**Bangladesh:** bangladeshadventistrms@gmail.com
**China:** Tel. & Fax: (+86) 24-2471 8125
ims1888@163.com
**India:** Cel.: (+91) 98-6203-0096
crosswell.rimsu@gmail.com
imsindia@rocketmail.com
**Indonesia:** Tel. & Fax: (+62) 21-860 7244
imssdarmjkt@gmail.com
annabelllgm@gmail.com
**Malaysia:** AsianDivision@sda1844.org
**Myanmar:** AsianDivision@sda1844.org
**Pakistán:** AsianDivision@sda1844.org
**Philippines:** Tel.: (+63) 32-269-1004
AsianDivision@sda1844.org
**South Korea:** Tel.: (+82) 2-220 1233
AsianDivision@sda1844.org
**Sri Lanka:** Tel.: (+94) 777-566 591
AsianDivision@sda1844.org

## PACIFIC

**American Samoa:** Tel.: (+684) 252 1870
sefoims_amsamoa@yahoo.com
**Australia:** Tel.: (+61) 2-9896 0150
OceaniaDivision@sda1844.org
**Cook Islands:** OceaniaDivision@sda1844.org
**Fiji:** Tel.: (+679) 3548477 / Cel.: (+679) 9533988
sanailaravia@yahoo.com
**New Zealand:** Tel.:0 (+64) 3-352 5023
OceaniaDivision@sda1844.org
**Papua New Guinea:** Cel.: (+675) 721 70 825
OceaniaDivision@sda1844.org
**Samoa:** Cel.: (+685) 7208011 / Cel.: (+685) 7249047
OceaniaDivision@sda1844.org

**INTERNATIONAL MISSIONARY SOCIETY**
**SEVENTH-DAY ADVENTIST CHURCH REFORM MOVEMENT**
**General Conference**

625 West Avenue • Cedartown, GA 30125 • U.S.A.
P.O. Box S • Cedartown, GA 30125 • U.S.A.
Telephone (+1) 770-748-0077 • FAX (+1) 770-748-0095
E-mail info@sda1844.org

---

**INTERNATIONAL MISSIONARY SOCIETY**
**SEVENTH-DAY ADVENTIST CHURCH REFORM MOVEMENT**
**TANZANIAN UNION**

P.O. Box 70908
Email: unoftzimssdarm@yahoo.com
Dar es Salaam Tanzania

biblewell.org

IMS
SDA CHURCH
REFORM MOVEMENT
THE FAITH OF JESUS

**www.asd1844.org**